

Hosea

Contents

Hosea

1Neno la Bwana lililomjia Hosea mwana wa Beeri wakati wa utawala wa Uzia, Yothamu, Ahazi na Hezekia, wafalme wa Yuda, na wakati wa utawala wa Yeroboamu mwana wa Yehoashi, mfalme wa Israeli.

Mke Wa Hosea Na Watoto

2Wakati Bwana alipoanza kuzungumza kupitia Hosea, Bwana alimwambia, “Nenda ukajitwalie mwanamke wa uzinzi na watoto wa uzinzi, kwa sababu nchi ina hatia ya uzinzi wa kupindukia kwa kumwacha Bwana.”³ Kwa hiyo alimwoa Gomeri binti Diblaimu, naye akachukua mimba na kumzalia Hosea mwana.

4Kisha Bwana akamwambia Hosea, “Mwite Yezreeli,¹ kwa kuwa kitambo kidogo nitaiadhibu nyumba ya Yehu kwa ajili ya mauaji ya kule Yezreeli, nami nitaukomesha ufalme wa Israeli.⁵ Katika siku ile nitavunja upinde wa Israeli katika Bonde la Yezreeli.”

6Gomeri akachukua tena mimba akamzaa binti. Kisha Bwana akamwambia Hosea, “Mwite Lo-Ruhama,² kwa maana sitaonyesha tena upendo kwa nyumba ya Israeli, kwamba nisije kabisa nikawasamehe.⁷ Hata hivyo nitaonyesha upendo kwa nyumba ya Yuda, nami nitawaokoa si kwa upinde, upanga au vita, wala kwa farasi na wapanda farasi, bali kwa njia ya Bwana Mungu wao.”

8Baada ya Gomeri kumwachisha Lo-Ruhama kunyonya, Gomeri alipata mwana mwingine.⁹ Kisha Bwana akasema, “Mwite Lo-Ami³ kwa maana ninyi si watu wangu, nami si Mungu wenu.

10“Hata hivyo Waisraeli watakuwa kama mchanga kando ya bahari, ambao hauwezi kupimika wala kuhesabiwa. Mahali pale walipoambiwa, ‘Ninyi si watu wangu,’ wao wataitwa ‘wana wa Mungu aliye hai.’¹¹ Watu wa Yuda na watu wa Israeli wataunganishwa tena, nao watamchagua kiongozi mmoja nao watakwea watoke katika nchi, kwa kuwa siku ya Yezreeli itakuwa kuu sana.

2“Waambie ndugu zako, ‘Watu wangu,’ na pia waambie dada zako, ‘Wapendwa wangu.’

Israeli Aadhibiwa Na Kurudishwa

¹ + 1:4 Yezreeli maana yake Mungu hupanda.

² + 1:6 Lo-Ruhama maana yake Sio mpenzi wangu.

³ + 1:9 Lo-Ami maana yake Sio watu wangu.

2“Mkemeeni mama yenu, mkemeeni,

k wa maana yeye si mke wangu,

n ami si mume wake.

A ondoe sura ya uzinzi katika uso wake

n a uzinzi kati ya matiti yake.

3Kama sivyo nitamvua nguo zake awe uchi

n a kumwacha uchi kama siku ile aliyozaliwa.

N itamfanya kama jangwa,

n itamgeuza awe nchi ya kiu,

n ami nitamuua kwa kiu.

4Sitaonyesha upendo wangu kwa watoto wake,

k wa sababu ni watoto wa uzinzi.

5Mama yao amekosa uaminifu

n a amewachukua mimba katika aibu.

G omeri alisema, ‘Nitawaendea wapenzi wangu,

a mbao hunipa chakula changu

n a maji yangu,

s ufu yangu na kitani yangu, mafuta yangu

n a kinywaji changu.’

6Kwa hiyo mimi Mungu nitaizuia njia yake

k wa vichaka vya miiba,

n itamjengea ukuta ili kwamba

a siweze kutoka.

7Gomeri atawafuatia wapenzi wake lakini hatawapata;

a tawatafuta lakini hatawapata.

K isha atasema,

‘ Nitarudi kwa mume wangu kama kwanza,

k wa maana nilikuwa na hali njema zaidi

k uliko sasa.’

8Gomeri hajakubali kuwa mimi ndiye

n iliyempa nafaka, divai mpya na mafuta,

n iliyemwongezea fedha na dhahabu waliyoitumia

k wa kumtumikia Baali.

9“Kwa hiyo nitachukua nafaka yangu wakati itakapokomaa

n a divai yangu mpya wakati itakapokuwa tayari.

N itamnyang’anya sufu yangu na kitani yangu

i liyokusudiwa kufunika uchi wake.

10Basi sasa nitaufunua ufisadi wake

m bele ya wapenzi wake;

h akuna yeyote atakayemtoa

m ikononi mwangu.

11Nitakomesha furaha na macheko yake yote:

s ikukuu zake za mwaka,

s ikukuu za Miandamo ya Mwezi,

s iku zake za Sabato,

s ikukuu zake zote zilizoamriwa.

12Nitaiharibu mizabibu yake na mitini yake,

a mbayo alisema yalikuwa malipo yake

k utoka kwa wapenzi wake;

n itaifanya kuwa kichaka,

n ao wanyama pori wataila.

13Nitamwadhibu kwa ajili ya siku

a lizowafukizia uvumba Mabaali;

a lipojipamba kwa pete

n a kwa vito vya thamani,

n a kuwaendea wapenzi wake,

l akini mimi alinisahau,” asema Bwana.

14“Kwa hiyo sasa nitamshawishi;

n itamwongoza hadi jangwani

n a kuzungumza naye kwa upole.

15Huko nitamrudishia mashamba yake ya mizabibu,

n ami nitalifanya Bonde la Akori ⁴

m lango wa matumaini.

H uko ataimba kama alivyofanya katika siku za ujana wake,

k ama siku zile alizotoka Misri.

16“Katika siku ile,” asema Bwana,

“ utaniita mimi ‘Mume wangu’;

h utaniita tena mimi ‘Bwana wangu.’

17Nitaondoa majina ya Mabaali kutoka midomoni mwake,

w ala hataomba tena kwa majina yao.

18Katika siku ile nitafanya Agano kwa ajili yao

n a wanyama wa kondeni, na ndege wa angani,

n a viumbe vile vitambaavyo ardhini.

U pinde, upanga na vita,

n itaondolea mbali katika nchi,

i li kwamba wote waweze kukaa salama.

19Nitakuposa uwe wangu milele;

n itakuposa kwa uadilifu na haki,

k wa upendo na huruma.

20Nitakuposa kwa uaminifu,

⁴ + 2:15 Akori maana yake ni Taabu.